

Jukumu la familia katika kuendeleza elimu jumuishi

Wazazi na wanafamilia kuwa na jukumu katika utetezi ili kuhakikisha ujumuishaji katika elimu kwa ajili ya watoto wao wenye ulemavu.

Wanafamilia wanaweza kusaidia ujumuishaji nyumbani, shuleni na katika jamii:



Nyumbani

- ✓ Wazazi wanapaswa kumtambua mtoto wao kama raia nmwenye haki kamili na majkumu. Ujumuishaji huanzia nyumbani.
- ✓ Wazazi na wanafamilia wa watoto wenye ulemavu wanaweza kuunda jukwaa jumuishi ambapo wanafamilia wote wanaweza kutoa msaada wao na kuelewa thamani ya ujumuishaji
- ✓ Kwa kuwatendea watoto/wanafamilia wao wenye ulemavu na wasio na ulemavu kwa usawa na kuwasaidia kushiriki katika shughuli za jamii kwa njia sawa, wazazi wanaweza kueneza thamani kubwa ya ujumuishaji katika jamii nzima. Hii pia inaunda kizazi kijacho cha advocates wa familia kati ya ndugu!



Katika jamii

- ✓ Wazazi na wanafamilia wanaweza kuunda jamii ya kieneo au kitaifa na majukwaa ambapo wanaweza kusaidiana na kubadilishana mawazo kuhusu jinsi ya kutetea ujumuishaji ndani na nje ya shule.
- ✓ Familia zinaweza kupata, kuwa sehemu, na kuimarisha mitandao ya usaidizi kwa ushirikiano na mashirika ya familia yanayoshughulikia haki za watu wenye ulemavu kuhusu elimu jumuishi.
- ✓ Wazazi na wanafamilia wanaweza kuchangia katika utungaji wa sera, sheria na miradi ili kujumuisha mtazamo wa ujumuishaji katika elimu kwa ushirikiano na serikali zao kwa lengo la kufanya mifumo ya elimu iwe jumuishi na kuleta mabadiliko ya kimfumo ya muda mrefu.
- ✓ Wazazi na wanafamilia wanaweza kuunda ushirikiano wa kimkakati na wahusika wakuu katika jamii zao, ili kudai elimu bora kwa wote bila ubaguzi.



Shuleni

- ✓ Wazazi na wanafamilia wanahitaji kujua kwamba mtoto/mwanafamilia wao hapaswi kamwe kunyimwa haki ya kupata elimu.
- ✓ Wazazi na wanafamilia wanatakiwa kujua haki na kanuni zilizopo nchini mwao kuhusu elimu na watu wenye ulemavu kwa ujumla.
- ✓ Wazazi na wanafamilia wanaweza kuchochea hitaji la elimu jumuishi, bora na yenye usawa.
- ✓ Wazazi na wanafamilia wanaweza kuunga mkono kujenga imani kati yao na walimu na maofisa wa shule, ili walimu na maofisa wa shule washiriki utalaam wao na washawishi maamuzi kuhusu elimu jumuishi kwa ajili ya watoto wao.



Shuleni

- ✓ Wazazi na wanafamilia wanaweza kuwasaidia walimu kuchangia katika kuondoa dhana potovu na ubaguzi dhidi ya watoto wenye ulemavu kwa kuwaeleza kwa nini elimu jumuishi hunufaisha wanafunzi wote.
- ✓ Wazazi na familia wanapaswa kuwa na imani kwamba wao ndio chanzo kikuu cha taarifa kuhusu watoto wao wenye ulemavu. Familia ndio wataalam katika kila kitu kinachohusiana na uwezo wa mtoto wao na usaidizi anaohitaji ili kufikia malengo yake na ni lazima wachangie maarifa hayo katika mazingira ya elimu.
- ✓ Wazazi na wanafamilia wanaweza kuwasaidia walimu na wakurugenzi wa shule kutambua rasilimali na usaidizi unaohitajika ili kuendeleza/kufanikisha/kuboresha ujumuishaji katika elimu.

Zamu yako: Wajibu wa Familia katika kusaidia Elimu Jumuishi

Je, ni njia gani nyingine unaunga mkono ujumuisho na elimu mjumuisho katika maisha ya mwanafamilia wako?



Nyumbani

.....

.....

.....



Katika jamii

.....

.....

.....



Shuleni

.....

.....

.....